
# 18 KITABU CHA UFUNUO NA HATIMA YA SAYARI YETU



Kutatokea nini juu ya sayari yetu hii katika mwisho wa dunia? Je, itatoweka? Kutatokea nini baada ya hilo? Sisi tutaishi wapi-kule mbinguni ama hapa duniani? Mungu aliiumba dunia hii ili ikaliwe na watu, lakini Paulo aliandika ya kwamba tutanyakuliwa mawinguni kwenda mbinguni (1 Wathesalonike 4:16, 17). Je, tutakuja kurudi tena duniani? Je, ni lini ambapo ile hukumu ya mwisho itakapofanyika na kutatokea nini kwa wale waovu? Je, watakuja kuadhibiwa? Kitabu cha Ufunuo kinasimulia juu ya vita dunia yote; hii itakuja kutokea wapi? Pia kinataja juu ya ile milenia, nayo ina mambo gani? Naye Shetani atakuwa wapi?

## *MWENDELEZO WA MATUKIO*

**1. Hivi leo yawezekana kuokoka. Tunaishi katika kipindi cha rehema. Je, ni kwa rai gani ambapo Mungu anawaambia wanadamu? Ufunuo 14:6, 7.**

_______________________________________________

*Katika Ufunuo 18:4, anatutaka tutoke katika Babeli ambayo inawakilisha yale machafuko ya kiroho ya wakati wetu huu.*

**2. Mara ule mlango wa rehema utafunga. Fursa zote za kuchagua njia ya Mungu zitafikia mwisho, Naye Kristo ataacha kufanya uombezi kwa ajili ya wanadamu. Ndipo kutasikika nini kutoka mbinguni? Ufunuo 22:11.**

*"Mwenye kudhulumu na azidi ________________, …na mwenye haki na azidi ______________ ."*

Kwa maneno mengine, hatima ya kila mtu itakuwa imetiwa muhuri, kwa ajili ya wokovu ama kwa kupotea.

**3. Je, kutatokea nini baada ya kipindi cha rehema kwisha? Danieli 12:1; Ufunuo 15:1.**

*Wakati wa ___________________, kumaanisha ___________________ mapigo ya mwisho.*

**4. Jina la ile vita ya kutisha itakayotokea katika lile pigo la sita ni lipi? Ufunuo 16:16.**

_______________________________________________

a) Mahali itakapopangiwa vita hii itakuwa ni katika Mashariki ya Kati, jirani na Yerusalemu.
b) Mataifa yote ya dunia yatahusishwa (Yoeli 3:9 -14).
c) Kutakuwako na umwagaji mkubwa wa damu (Ufunuo 14:20).
d) Vita hii itakuwa pia itakuwa ni pambano kati ya Shetani pamoja na wafuasi wake dhidi ya Kristo na watu Wake.
e) Ni nani atakayeshinda katika vita hii? Kristo atakuwa ni mshindi mkuu (Ufunuo 19:13-16).

## *MATUKIO MWANZONI MWA ILE MILENIA*

**5. Je, ni tukio lipi litakaloashiria mwisho wa dunia na mwanzo wa kile kipindi cha miaka elfu moja? Ufunuo 14:14-16.**

__________________________ *wa pili wa* ______________________________.

- Kila jicho litamwona (Ufunuo 1:7), na kila sikio litamsikia (1 Wathesalonike 4:16).
- Mbingu itakunjwa kama ukurasa ukunjwavyo, na visiwa vitaondolewa kutoka mahali pake (Ufunuo 6:14).

**6. Baada ya tetemeko kubwa la nchi, ni nini kitawatokea wale waliokufa katika Kristo? Ufunuo 16:18; 1 Wathesalonike 4:16. ______________________________**

- Wale wanaofufuliwa katika ufufuo huu, wanaitwa wenye heri. Ufufuo 20:6.

**7. Kutatokea nini kwa wale waliofufuliwa na wenye haki walio hai pale Yesu ajapo? 1 Wathesalonike 4:17.**

*Watabadilishwa na kuwa katika kutokufa (1 Wakorintho 15:51-54) na ____________________ katika mawingu. Wenye haki watasafiri katika anga hadi kunako makazi ya mbinguni ambako watatawala pamoja na Kristo kwa miaka elfu.*

**8. Kutatokea nini kwa waovu walio hai bado pale Yesu ajapo? 2 Wathesalonike 1:7-9.**

______________________________________________________________

*Waovu waliokufa watabaki kuwa wafu.*

## *MATUKIO KATIKA ILE MILENIA*

**9. Kutatokea nini kwa Shetani? Ufunuo 20:1-3.**

*Shetani atafungwa kwa miaka ________________________________.*

*Hatafungwa kwa dhahiri bali atafungwa kwa mazingira ambayo hatakuwa na mtu wa kumdanganya maadamu waovu watakuwa wamekufa na wale wenye haki watakuwa mbinguni. Ndivyo kipindi hiki kitakavyokuwa kwa Shetani.*

**10. Dunia itakuwa kama nini katika ile miaka elfu moja? Yeremia 4:23-27.**

______________________________________________________________

*Ni nini kitaifanya dunia kuwa ukiwa?*

- Yale mapigo saba yatakuwa yameharibu sana.
- Har Magedoni itawaacha wengi kuwa wafu. Yeremia 25:33; Isaya 24:22.
- Lile tetemeko kuu la nchi la pigo la saba litaharibu miji mikuu yote ya dunia.
- Ujio wa Kristo kati ya miale ya moto utakamilisha maangamizi. 2 Wathesalonike 1:7, 8.

**11. Je, wale watakatifu (waliokombolewa) watafanya nini kule mbinguni? Ufunuo 20:4.**

______________________________________________________________

- Watatathmini adhabu ambazo zinawastahili wale waovu. 1 Wakorintho 6:2, 3.
- Haki ya Mungu itadhihirika kwa njia ya kushiriki kwa watakatifu hawa katika hukumu.

## *MATUKIO MWISHONI MWA ILE MILENIA*

**12. Yesu atakuja katika dunia hii baada ya ile miaka elfu. Ni nani watakaoambatana Naye? Zekaria 14:4-6. ________________________________________**

*Toleo la Straubinger linasema, "Katika siku ile hapatakuwa na nuru, ni baridi pekee pamoja na theluji." Zekaria 14:6.*


**13. Mtume Yohana aliona nini kikishuka kutoka mbinguni? Ufunuo 21:2.**

______________________________________________________________

**14. Je, kutatokea nini kwa wengine waliokufa (waovu)? Ufunuo 20:5. ______________**

**15. Kutatokea nini kwa Shetani? Ufunuo 20:7.** *Ata______________ kutoka katika gereza lake.*

a) Mazingira yale yaliyomfanya kuwa mfungwa yatakuwa yametoweka, kadiri vile kutakuwako na watu wa kuwadanganya.


MIAKA ELFU MOJA
HUKUMU
MBINGUNI
Ufufuo wa wenye haki
Waovu wafu
Kuokolewa kuhamishwa
KUJA KWA PILI
Ufufuo wa waovu
Shetani aliachiliwa
Shetani na waovu kuharibiwa
DESCIENDE LA NUEVA JERUSALÉN
HOY
SATANÁS ATADO
ETERNIDAD

b) Udanganyifu mkubwa utafanyika. Ufunuo 20:8, 9.

- Shetani atawahakikishia kwamba yeye ndiye aliyewafufua.
- Atawaambia kwamba wataweza kuuteka ule mji wa Mungu na kuweka ufalme wa kwao wenyewe.

c) Katika wakati ule, kile kiti kikuu cha enzi pamoja na Hakimu wa ulimwengu wote akiketi juu yake, wataonekana. Ufunuo 20:11.

- Kila mwanadamu atayaona maisha yake mwenyewe, kama vile filamu, yakipita mbele ya macho yao.

**16. Je, ni kitu gani kitashuka kutoka mbinguni pale Shetani pamoja na wale waovu watakapojaribu kuushambulia mji ule? Ufunuo 20:9.** ______________________________

a) Ile hukumu itakuwa kwa kulingana na kila mtu anavyostahili. Ufunuo 20:13.

b) Mauti ya pili itakuwa ndio ya mwisho. Ufunuo 20:14, 15.

c) Hapatakuwa na shina wala tawi lililoachwa. Kutabakia majivu pekee, jambo ambalo linamaanisha ya kwamba katika kiwango fulani ule moto utazimishwa. Malaki 4:1-3.

**17. Je, Mungu atafanya nini na dunia baada ya kutakaswa kwa njia ya moto? 2 Petro 3:11-13.**

______________________________________________________________________

a) Waliokombolewa wataishi kwa furaha katika dunia mpya kwa milele. Ufunuo 21:3, 4.

b) Mpango wa Mungu wa kurejesha utulivu wa paradiso ya Edeni utatimilika.

## *HITIMISHO*

- Je, wewe utakuwa wapi katika ile miaka elfu - kule mbinguni ama duniani?
- Utakuwa wapi mwishoni mwa milenia-katika Yerusalemu mpya ama miongoni mwa wale watakaoangamia kule nje?
- Katika ule umilele wewe unapanga kuwako wapi?
- Yesu amefanya kila kitu kwa ajili yako. Anataka kukuokoa. Je, utamruhusu afanye hivyo?

*__Uamuzi wangu:__ Ninaamini juu ya maisha ya milele na ya kwamba Mungu atafanya nchi mpya baada ya ile miaka elfu.* ◯ *Ndio* ◯ *Hapana*

**Matukio ya mwisho kwa ufupi:**

| WAKATI WA MWISHO | Ufufuo wa kwanza | MIAKA 1,000 | Ufufuo wa pili | UMILELE |
|---|---|---|---|---|
| Wakati wa rehema | | Kule mbinguni: watakatifu wahusika katika Hukumu | | Ujio tatu wa Kristo |
| Mapigo Saba-Har Magedoni | | | | Yerusalemu Mpya Unashuka toka mbinguni |
| Kuja mara ya pili kwa Kristo | | | | |
| Ufufuo wa kwanza wa watakatifu | | Waovu Wamekufa | | Ufufuo wa pili (wa waovu) |
| Kubadilishwa na kunyakuliwa | | Shetani amefungwa | | Shetani amefunguliwa |
| Kuuawa kwa waovu | | Nchi imekuwa ukiwa | | Udanganyifu wa Mwisho |
| | | | | Moto kutoka mbinguni |